
*jarida la kila mwezi*

# NGURUMO ya mwandishi

TOLEO LA XXV
OKTOBA MMXXIII



## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Mwaka wetu wa tatu huoooo…—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Hussein Omary Molito— Uk 03

**New In Town:** Ujumbe wa Abdulrazak Gurnah**—**04

**PITIO LA VITABU**— Gamba la Nyoka (Ikisiri) 4—Uk 05

**MAKALA**— SAIKOLOJIA: Hakuna Ulichopoteza —Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji '10'— uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Samora Machel '9'— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Simulizi Club **—**Uk 11

**RIWAYA:** —Kisasi cha Hisia '01'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '8'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Aladini na Wezi 40 '4'- Uk 16

**HABARI/MATANGAZO** – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Zijue maktaba 10 bora duniani —Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** Peponi —Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO—** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**ELIMU JAMII:** Unaijua mimea inayokula nyama? **-** Uk 23

**NGURUMO YA MWANDISHI**

***©RICHARD MWAMBE***

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0628124486**
**WhatsApp: +255 766974865**

**jamvilasimulizi@gmail.com**

## TAHARIRI: Mwaka wetu wa tatu huoooo…

Wasalaam,

Ni furaha kubwa kwa mara nyingine kuwaambia kuwa sasa tnaianza safari ya mwaka wa tatu. Ngurumo ya Mwandishi limekaa hewani kwa takribani miezi 24 bila kukosa ukiachana na changamoto ndogondogo za kiutendaji.

Kwakweli tunamshukuru Mungu, na tunawashukuru wote ambao wamekuwa wakitupatiaa makala na maandiko anuai ili kuweka katika jarida hili na kuwapa elimu na burudani wasomaji wetu. Nyote tunawashukuru sana, mnajitoa kwelikweli katika kufanikisha hili. Bila ninyi tungefika wapi?

Tulipoanza kutoa jarida pepe hili, kazi haikuwa rahisi maana watu wengi hawakulielewa au kulipokea vyema. Lakini kadiri tunavyoendelea wasomaji wengi wamejitokeza hata mara kadhaa kupiga simu na kuuliza 'linatoka lini', hii inatupa moyo sana wa kuendelea mbele.

Siwezi kuwataja mmoja mmoja lakini ni wengi mmetufikisha hapa tulipo. Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru na wale ambao wanaweka matangazo yao ya biashara kwani kupitia hayo pia tumeweza kupata chochote ambacho kimetusogeza hatua moja mbele. Mbarikiwe na Bwana.

Napenda tu kuwaambia kuwa katika mwaka wetu huu wa tatu tumewaongezea vitu kidogo. Tumeongeza safu ya MALENGA WA KILEO; huu ni uwanja wa wale washairi kujimwayamwaya, karibuni sana sasa tunapokea mashairi. Pia tumeongeza safu ya ELIMU JAMII ambayo kwayo itakuwa kama darasa kwa wasomaji kujifunza mambo mbalimbali yatayowakwamua kiuchumi au hata kiakili. Lakini pia tumewekaa safu ya mapichapicha eenh, HABARI PICHA; usishangae ukajikuta kwenye safu hiyo umeng'aa, kaa chonjo.

Ni matumaini yetu mtatupa sapoti sana katika hatua hii ya tatu muhimu ili tufike kule tunakotaka. Nyote mnakaribishwa sana kuleta Simulizi, Makala za kifasihi au za kutoa elimu, mashairi na tenzi, matangazo ya biashara na vingine vingi.

Twawakaribisha sana sana sana, mjisikie mko nyumbani. Na ninyi waandishi Abdulrazak Gurhan anakuambieni "Msiache kuandika… ipo siku"

**Richard Mwambe**
**CEO-Ngurumo ya Mwandishi**

# MWANDISHI WETU: HUSSEIN OMARY MOLITO

**Katika safu yetu ya MWANDISHI WETU, leo tunaye mwandishi maarufu, machachari mwenye mvuto na watu na anayejua kuitumia kalamu yake kutoa burudani. Si mwingine bali yeye mwenyewe atajieleza.**

Naitwa Hussein Omary Molito. Ni mtoto wa tano kati ya watoto saba kwa baba yangu. Ni mtoto wa tatu kati ya watoto wanne kwa mama yangu.

Mwanzo nilikuwa na ndoto ya kuja kuwa mchoraji mkubwa, nilishapokea tuzo ya uchoraji nilipokuwa  darasa la tano. Kusoma vitabu ilikuwa moja ya starehe yangu toka nipo darasa la tatu.

Nilibahatika kusoma shule yenye maktaba. Na kusoma ilikuwa ndani ya ratiba kabisa kwenye masomo yetu.
kipaji cha kusimulia kilianza kuonekana kwanza kabla ya uandishi. Nikiwa darasa la tano, nilikua na uwezo wa kusoma kitabu na kukikariri, na kusimulia hadithi ya kitabu mbele ya darasa.
Nilipofika darasa la saba, nilipewa dhamana ya kutunga maigizo. Na hapo ndipo utunzi ulipoanzia.

Hadithi yangu ya kwanza ilitoka kwenye gazeti la Alasiri mwaka 2006 na kuniaminisha kuwa naweza kutunga.
2007 Nikajiunga na kikundi cha maigizo kilichoitwa SHIRIKISHO MSANII AFRIKA. Kipindi hiki nilikuwa naonekana kupitia stesheni ya ITV. Ikanifanya niwe maarufu shuleni.
Nilipofika kidato cha tatu, ikanibidi niache kila kitu ili nifocus na masomo.
Uchoraji, kuigiza, uandishi nikavizika hapo hadi mwaka 2011.

Hapo nikachagua uandishi na nikaanza kuandika tena na kutuma huku facebook. Kipindi hiki watumiaji wa mtandao huu nchini tulikuwa wachache sana.
2012 nikaomba kujiunga na Group linalomilikiwa na Frank Masai. Tukawa tunapost hapo hadithi.

2014 nikawa maarufu. Wasomaji wa mtandaoni kipindi hicho wakanikubali. Maandishi yakaanza kuwa biashara. Mashabiki walichanga pesa na kufanikiwa kutoa kitabu changu cha kwanza nilichokiita MAPIGO YA MOYO. Hiki nilikuja kushoot hadi movie yake 2016.
2019 nikatoa kitabu cha kwanza kikubwa chenye ISBN. Hapo ndipo nikahesabiwa kama mwandishi ninayejulikana kwenye kumbukumbu za maktaba kuu.
Tarehe 3/July mwaka jana nimetoa kitabu cha Kumi. Ila ndo kitabu cha kwanza kuzinduliwa mbele ya nguli mbalimbali kwenye tasnia hii.

Kitabu cha CHAWA ndicho kitabu nilichowekeza pesa nyingi. Sikuwahi kuchapa nakala 500 kitabu chochote kile, ila hiki nimechapa nakala 1,500.

**VITABU NILIVYOTOA**
-SIKU 71 (2019)
-KAULI YA MWISHO (2019)
-KISIWA CHA WANAWAKE ( 2019)
-SAYARI NYEKUNDU (2020)
-IZARA (2020)
-ALICE THE SUPER STAR (2020)
-SEKELA (2021)
-LAITI KAMA (2021)
-TYPHIN (2021)
-CHAWA (2022)

Mwaka 2023 sijatoa kitabu chochote kipya zaidi ya kuchapa tu nakala zilizopita. Mwakani tukijaaliwa uhai nitarudi sokoni na vitabu zaidi ya viwili.

Mwisho nawashukuru tu wasomaji wa vitabu, mbali na changamoto nyingi zilizopo kwenye tasnia yetu, wanatuvumilia na kutuelewa. Huwa naumia sana ninapomtoza hela ya basi mtu wa nje ya mkoa wa Dar ili apate kazi yangu. Natamani vitabu vyangu viwepo kila mahali, wanunuzi wanunue kwa bei sawa popote walipo ndani na nje ya Tanzania. Nawasihi tu wasituchoke, tunaelewa na tunalifanyia kazi hili kadri tunavyoweza!

Nishukuru tu uongozi wa ukurasa huu kwa kunipa nafasi hii adhimu.
Ahsante!

**NGURUMO YA MWANDISHI linakutakie heri na baraka nyingi na mafanikio katika uandishi wako.**

Penda kusoma vitabu

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

## UJUMBE WA ABDULRAZAK GURNAH, MSHINDI WA TUZO YA NOBEL 2021 KWA WAANDISHI

MWEZI wa Novemba ulikuwa wenye faida sana kwa waandishi na wasomaji wa vitabu nchini Tanzania, hususan Dar es salaam.

Kitabu PEPONI kilichoandikwa na mwandishi nguli, mwenye Tuzo ya Nobel, Abdulrazak Gurnah ambacho kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Ida Hadjivayanis kilizinduliwa.

Tukio hili lilifanyika pale Alliance Francaise jijini Dar es salaam na kuhudhuriwa na waandishi pamoja na wapenzi mbalimbali wa fasihi nchini.

Abdulrazak Gurnah Mtanzania anayeishi huko Uingereza alikuwapo mwenyewe na kupata nafasi ya kusaini baadhi ya vitabu vilivyonunuliwa siku hiyo. Hakuishia hapo bali aliacha ujumbe kwa kizazi chote cha waandishi. Anasema:

**"Ukitaka kuandika lazima uwe na haja, kuna kitu ambacho kitakulazimisha uandike. Kwasababu kazi hii ya uandishi ni ngumu, ngumu kwa sababu mnajua… najua hapa wengi ninyi ni waandishi… ngumu kwa sababu unaandika. Unajitahidi we mwenyewe lakini hupati mtu ambaye atapiga chapa hilo buku lako.**

**Hata ukibahatika mtu akataka kupiga chapa, hakuna mtu anataka kusoma hilo buku lako. Na unaandika jingine, na unaandika jingine. Utachoka na utasema aaaagh, napoteza wakati wangu bure tu, bora nifanye kitu kingine.**

**Lakini, ukiwa una haja, ikiwa kuna kitu kinakulazimisha utaendelea tu. Kwahivo ikiwa kuna baadhi yenu hapa ambao mnaanza kuandika au mmeandika kwa miaka hivi, na bado watu hawajui maandishi yako, hawakusifu, usiogope, itakuja siku yoyote".**


**Na hivi ni baadhi ya vitabu alivyoandika**

Paradise (Peponi) -1994 (kimetafsiriwa Kiswahili)
After Lives -2020
Desertion -2005
By The Sea -2001
Memory Of Departure -1987
The Last Gift -2011
Gravel Heart -2017
Admiring Silence -1996
Pilgrims Way -1988
Dottie -1990
Last Gift -2014

**Historia fupi**

Abdulrazak Gurnah ni Mtanzania wa kuzaliwa, mwandishi wa vitabu kutoka Uingereza, aliyetunukiwa Tuzo ya Nobel katika fasihi mwaka 2021. Amezaliwa Zanzibar wakati wa utawala wa Sultan na miaka ya 1960 walihamia Uingereza kama wakimbizi wakati wa vuguvugu la Mapinduzi.

Amezaliwa tarehe 20 Disemba, 1948 huko Zanzibar. Amesoma Chuo kikuu cha Cantebury Christ Church na Chuo Kikuu cha Kent



# KITABU: GAMBA LA NYOKA –Ikisiri (4)

Tunaelezwa:

Mawazo haya yalimsumbua sana kichwani kiasi cha wapanda baiskeli  kumpigia kengele mara nyingi na kumtukana alipochelewa kuwapisha.

Lakini mwishowe alianza kujilaumu mwenyewe. Alipokuwa Mwenyekiti wa kijiji, pesa nyingi zilipita na kutua mikononi mwake. Alianza kufikiri jinsi alivyozitumia ovyo; akajuta (uk. 99).

Maelezo haya yanamdunisha Mambosasa kiasi cha kumfanya kiumbe cha kuhurumiwa, hasa anapojutia maovu yake. Kisa kinaendelea kusimulia jinsi rais anapotua uwanja wa ndege, Mambosasa anapuuzwa na waandalizi wa sherehe kwa sababu hawamtambui. Baada ya sherehe fupi ya kumkaribisha kiongozi wa taifa, tangazo linatolewa kusema kwamba rais ataondoka kwenda kwa gari kwenye uwanja wa sherehe hasa. Tunaelezwa jinsi Mambosasa anavyotumia hila ili awahi kwenye uwanja wa tafrija kwa maneno yafuatayo:

Badala ya kujidai mtu mkubwa na mheshimiwa, alikata shauri kutenda matendo ya kiuanafunzi. Alikumbuka fujo zake za zamani pale Chuo Kikuu, jinsi alivyokuwa akiingia kwenye tafrija za walimu na kunywa kwa fujo na matusi juu ya walimu (uk.102).

Kwa kuongozwa na mawazo haya potovu, anadandia gari linalowapeleka wenyeviti wa vijiji. Wanapofika, Mambosasa anajipenyeza hadi kwenye ukumbi wa tafrija. Inachekesha sana anavyogunduliwa na askari wa kike wa jeshi la kujenga taifa wakati anavuta kiti na kukaa. Askari anamwambia kwa ukali:

"*Wewe si mgeni! Tunaogopa tu kukufukuza mbele ya rais. Kaa lakini usirudie tena safari nyingine!"* (uk.103). Mambosasa anapopata fursa baadaye, anakunywa pombe na kulewa. Halafu la kuchekesha zaidi ni kwamba anapolewa, anakusanya makombo, kuyatia kwenye bahasha kubwa na kuyapelekea familia yake. Mkewe anamkaripia vikali na kuyatupa. Jambo linalozidisha bezo juu ya mhusika huyu ni jinsi alivyo kigeugeu. Mara tunamuona akijutia makosa yake; lakini punde si punde anafanya mengine ambayo ni ya kitoto – kama tulivyoona hapo juu.


### 3.0 Mama Tinda na Padri Madevu

Tunawachunguza wahusika hawa kwa pamoja kwa sababu uumbaji wao kwa kutumia tashtiti unategemea uhusiano kati yao kwa kiwango kikubwa. Jambo hili litabainika katika maelezo yanayofuata. Mbinu ya kitashtiti inayotumiwa katika riwaya kumchora Mama Tinda ni ucheshi.

Vitendo vyake anapoenda kanisani kuabudu vinaibua kicheko hasa kutokana na uelewa wake mdogo wa dini ya Kikristo. Jambo linalomsumbua mama huyu na linalomsukuma kwenda kanisani kumuomba Mungu amsaidie kukabiliana nalo linahusu tishio la kubomolewa kwa nyumba yake. Maofisa wanaotekeleza sera ya kuhamishia watu kwenye vijiji vipya wamemuonya kwamba nyumba yake iko nje ya kijiji kipya anachotakiwa kuhamia kwa sababu hii itabomolewa.

Analipinga sana jambo hili na hataki nyumba yake ibomolewe. Mama Tinda akiwa peke yake kanisani mkabala na sanamu za Yesu, Maria na kiwakilishi cha Utatu Mtakatifu, anaanza kwa kuikabili sanamu ya Yesu na kuomba kama ifuatavyo:

## PITIO LA VITABU




*Yesu! wewe ni Mungu. Ulizaliwa na mwanamke kama mimi. Mimi ni mama yako…Wewe uliyewachapa Wahindi kwa kuuza bidhaa zao ndani ya nyumba ya Baba yako, okoa nyumba zetu. Wachape  hao watakaozibomoa* (uk. 2)

Ombi hili linachekesha kwa sababu ya mtindo wake usiokuwa wa kimaombi. Linajitokeza kama maelezo ambayo Mama Tinda anatoa kwa binadamu mwenzake.  Pili, yanaonesha kutoelewa mambo ya kimsingi kuhusiana na Ukristo, hasa kuzaliwa kwa Yesu na kitendo chake cha kuwafukuza hekaluni watu waliokuwa wakifanyia biashara humo.

***Je unataka kuisoma yote Ikisiri hii? Whatsapp 0766974865***

# -SAIKOLOJIA-
# HAKUNA ULICHOPOTEZA

**Madam**
**Neema Mbilinyi Mgao**



## HAKUNA ULICHOPOTEZA.

**MAKALA HII NI MAALUMU KWA WALE WOTE WALIOPITIA CHANGAMOTO MBALI MBALI HATA WAKAJIKUTA WAMEANZA UPYA.**

Umepata nafasi ya pili ya kuishi? Ulikua na afya nzuri na ghafla ukapata changamoto za kiafya zilizopelekea mwili na muonekano wako kwa ujumla ukawa sio ule uliozoeleka? Nini kimekupitisha katika mateso hadi umejikuta umepoteza karibu kila kitu kwenye maisha? Unajihisi na kujiona kuwa umepoteza mwili au mali? Haujapoteza.

Ndiyo,haujapoteza. Ni sawa, umepitia mitihani kwamba ulikua imara kiafya, lakini eidha umeumwa maradhi yaliyokufanya upoteze nuru au mvuto wako au pengine ulikua na maisha mazuri. Kwako ndiyo vile watu waliita mboga saba, meza ya kulia chakula kwako ilifanywa iwe meza ya kucheza mchezo wa *draft,* kwa maana ya ugali kidogo, ila mboga nyingi. Ni sawa, maisha yalikua bora, lakini kwa kudra za Mungu afya imeteteleka, uchumi umeyumba na mengine mabaya yanakuandama. Lakini ikiwa leo umepata nafasi ya kusoma andiko hili na hiyo hali uliipitia eidha wewe mwenyewe au jamaa yako alipitia basi nikuombe tuu ujue kwamba haujapoteza.

Mara chache sana binadamu huwa tunapata nafasi ya pili ya kurekebisha mfumo mzima wa maisha yetu hasa pale tunapopitia anguko katika maisha kwa ujumla, anguko linapotokea ni nadra sana mtu kulipokea kwa uharaka, wengi huangukia kwenye kutenda matendo ambayo hawakua wakiyatenda, mathalani kuangukia kwenye ulevi, tabia ambayo mtu hakua akiifanya lakini anajikuta anaianza ili kujifariji katika anguko hilo.

Maisha ya kila siku yana siri sana, yanakutaka mwanadamu kuvumbua mambo mapya na kuyafanya kiukamilifu au basi uyafanye kiukamilifu yale ambayo unaona ni wazi kwaamba yanakuletea faida. Yasiyokuletea faida achana nayo kwa uwepesi.

**KWANINI MTU UHISI KUPOTEZA.**

Zipo sababu nyingi ambazo mtu akizipitia au zikimtokea moja kwa moja atahisi au atajishuhudia kuwa amepoteza kila kitu kwenye maisha yake, tuone baadhi.

**1). Kuchekwa.**

Mchukue mtu aliyekua na maisha mazuri sana, na watu iwe ndugu au jamaa wakajua kuwa ana maisha mazuri, ghafla akaanguka kiuchumi yaani uchumi ukayumba. Huyu anapopitia wakati huu na akaona anachekwa basi kwanza humletea kusononeka na kuhisi kujidharau na hata kuona amepoteza kila kitu kwenye maisha yake.

Mathalani mtu amepitia homa sana, niseme alikuwa na pengine uzito wa kg 104. Si unajua mtu kwa uzito huo anakua na mwili mkubwa. Ghafla akapata shida ya kiafya, mpaka kupona akajikuta anakua na uzito wa kg 60, halafu pengine kuna mtu aliyekua akimfahamu kwenye ubora wake na leo akakutana nae mwili ukiwa umeisha. Ile hali mtu ya kumuonesha kushangaa pengine hata kwa kuuliza, basi moja kwa moja mtu huyu atajihisi amepoteza mvuto wake na atasononeka.

**2). Kutengwa.**

Ikiwa mtu aliyepitia maradhi au kuporomoka kiuchumi akashuhudia kutengwa eidha na familia au na watu wa nje ya familia pia inaweza kumfanya mtu akaona moja kwa moja kuwa amepoteza.

**TIBA YA HALI HII YA KUJIHISI KUPOTEZA.**

Kisaikolojia mtu aliyepitia mitihani yoyote, iwe ya maradhi au ya kiuchumi, akaipata hiyo hali ya kuhisi kupoteza, basi huyu moja kwa moja saikolojia yake haitokua sawa. Atakumbwa na sonona, atakumbwa na upweke, atakumbwa na kukataliwa, na mengine yote mabaya ambayo pengine wenzie hawawazii hayo yeye yatamkumba.

# -SAIKOLOJIA-
# HAKUNA ULICHOPOTEZA

**Afanye nini basi.**
Tiba kubwa ya Saikolojia ya mtu anayo mtu yeye mwenyewe. Yaani mimi ndio tabibu mkuu wa hali yoyote ile itakayonikumba kisaikolojia. Mimi kwanza najitibiaje kabla ya kupata msaada wa mwingine.

**a). Pokea matokeo.**
Moja kati ya tiba za hali hiyo, hali ya kujihisi kupoteza, ni kuyapokea matokeo. Hii ni hatua moja kubwa na nzuri mno katika mfumo wa maisha kila siku. Sema na moyo wako, kama umetoka kwenye kuumwa saana, mwili ukaisha basi kwanza kubali kuwa wewe uliumwa na kwamba kila aliyeumwa ni lazima kupungua mwili. Hakuna mtu aliyeumwa akanenepa. Kubali kuwa kuumwa ni hatua ambayo kila aliye na pumzi ataipitia. Kubali kwamba tunatofautiana nyakati tuu za kupitia lakini kubali kuwa ni lazima kupungua. Kubali ni lazima kufirisika, kubali kwamba hauwezi kudumu na hali nzuri kila siku, kwamba kama maisha ni lazima kupanda na kushuka. Hiyo ndiyo kanuni ya maisha ya kila siku, ipokee.

**b). Anza upya.**
Kama umepata nafasi ya pili, maana kuna walioumwa na wakaikosa nafasi ya pili ya kuishi (wakafariki), kuna waliofilisika wakashindwa kuipokea ile hali, ni eidha walikufa au walijiua na kuikosa nafasi ya pili. Ikiwa wewe umepata nafasi ya pili basi anza upya. Anza upya kuyaishi hayo maisha ambayo unaendelea nayo. Kama haujaumwa kwa kiwango cha kupoteza macho, mikono, miguu basi anza upya. Usiogope kuanza upya.

**c). Usiogope.**
Wewe ndiyo maana halisi ya wewe mwenyewe, yaani wewe ndio wewe hivyo usiogope wala kumfikiria mwingine. Kama nilivyosema,tabibu mkubwa wa moyo wako ni wewe mwenyewe. Tabibu mkubwa wa akili yako ni wewe mwenyewe, maisha yako ni wewe mwenyewe, hivyo usimuogope mtu, usimfikirie mtu, wewe ishi vile unavyoweza kuishi. Usimhofie mtu. Wakikutazama unavyoishi jiambie "kama wanaakili watajifunza".

**d). Jiongeleshe.**
Ndiyo, jiongeleshe wewe binafsi, na sio tuu kujiongelesha bali jiongeleshe mambo mazuri, mfano "ipo siku nitainuka tena," "maadamu nipo hai basi hakuna nilichopoteza" na mengineyo mazuri jisemeshe.

**e). Mshukuru Mungu.**
Unaweza sema nimekosea kupanga mtiririko wa tiba hii, lakini la! Sijakosea. Mungu anashukuriwa kila wakati, na kila muda, lakini nikuulize, haujawahi kupitia wakati mgumu kiasi cha kujiuliza "hivi wewe Mungu upo kweli?" Yaani haujawahi kupitia wakati mgumu kiasi cha kumkufuru Mungu? Sasa kama jibu ni umewahi basi utaelewa kwanini hii ni hatua ya mbali hivi. Shukuru Mungu kila wakati, na umuombe msamaha kwa kumkufuru, lakini hatua hii itenge ijitegemee. Shukuru Mungu. Mpaka Mungu amekupa nafasi ya pili ni kwakuwa wewe u wa thamani. Sasa mtengee nafasi yake ili kumshukuru katika nyakati hizo ulizopitia. Mshukuru na muombe kila wakati huyu Mungu.

**f). Endelea kujiimarisha.**
Endelea kujiimarisha kufanya hicho unachofanya katika nafasi yako ya pili ya maisha yako. Kumbukumbu zikukumbushe kuwa kunawalioshindwa kufanya kwa kukosa nafasi ya pili ya kufanya. Hivyo wewe kama umepata nafasi ya pili, umeinuka upya basi endelea kujiimarisha kufanya hicho unachofanya katika nafasi ya pili ya kuishi.

Hatua hizo na zingine utakazovumbua maana kumbuka nimesema tabibu mkubwa wa moyo na Saikolojia yako ni wewe mwenyewe, basi vumbua njia chanya za kufanya ili kuzidi kujiimarisha katika mfumo wa maisha yako. Usikate tamaa, fanya mengi kwa kuwa Mungu amekuzawadia nafasi ya pili. Kwa imani yako endelea kumuomba Mungu na hata wewe unaeona mbona hauna mtihani wowote usiache kumuomba Mungu. Tunamhitaji Mungu kila wakati.

---

**Karibu kwa mazungumzo mengine ya kisaikolojia na kwa ushauri pia.**
**Asante.**

**Madame Neema Mbilinyi Mgao,**
**Kisasa,**
**Dodoma,**
**Tanzania.**
**What's app no. 0746-139654.**

# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-10



Na. Ramadhani Makoleko

**Nyumba nzima ilitawaliwa na vilio. Kila mtu alisema lake. Huyu alisema hivi na yule alisema vile. Wengi walitaka kujua kilichomuua. "Yaani hakuumwa hata kidogo," jirani mmoja alisema huku mwingine akisema amekufa angali msichana mdogo.**

Hakuna aliyekuwa na majibu zaidi yangu. Hata hivyo, sikuthubutu kumwambia mtu. Mama hakuwezekana, shangazi naye alikuwa hoi. Baada ya maiti kuingizwa ndani, wanafamilia walikutana kupanga taratibu za mazishi. Walipigiwa simu kaka na dada ambao walisema asizikwe mpaka wafike. Ilikuwa ngumu kutokana na hali ya maiti kwani mara tu baada ya kuingizwa ndani ilianza kuvimba.

Kwa namna ilivyokuwa inavimba kila wakati ilikuwa ngumu kumchelewesha kuzikwa. Kikao kile kiliafikiana azikwe kesho yake saa nne asubuhi. Wakati hayo yakiendelea, nilikuwa sijaushuhudia mwili wa marehemu. Japo nilipenda kufanya hivyo, lakini niliogopa. Kila nilipotaka kufanya hivyo moyo wangu ulisita.

Maiti ilishughulikiwa. Msimamizi mkuu wa kuishughulikia alikuwa shangazi na rafiki yake marehemu. Watu wachache walikuwa chumbani huko wakifanya hiki ama kile mpaka walipomaliza kumuandaa marehemu. Walipomaliza ndugu, jamaa na marafiki waliruhusiwa kwenda kumshuhudia. Walianza baba na baba yake shemeji. Kisha alifuatia mama na ndugu wengine. Baadaye kabisa niliingia.

Niliingia chumbani nikiwa na wasiwasi mkubwa. Wasiwasi huo sijui ulitokea wapi. Nilijipa moyo nikaingia. Niliwakuta shangazi na rafiki wa marehemu wakiwa pembeni ya mwili wa marehemu. Rafiki wa marehemu aliponiona alinifuata akanishika mkono. Aliniongoza hadi kwenye kitanda ulipo mwili wa dada. Tulipokifikia kitanda rafiki wa marehemu alifunua shuka ili kunionesha mwili wa marehemu. Ajabu alipofunua shuka, sikuona kitu chochote zaidi ya kunguru ambaye alikuwa amefunikwa na ile nguo ya ndani. Nilishtuka hata nikapiga kelele.

"Mamaaaa!" Rafiki wa marehemu aliniwahi akanituliza. Alidhani nimeshtuka baada ya kuuona mwili wa marehemu. Haikuwa hivyo. Alinituliza. Wakati huo aliufunika ule mwili wa marehemu. Nilikaa chumbani huko kwa muda kisha alinitoa nje. Moja kwa moja hadi chumbani kwa mama ambako nilimkuta mama na mama yake shemeji na watu wengine wakibembelezana. Niliungana nao katika kuomboleza. Kichwani nilikuwa na mawazo mengi sana. Mawazo yangu yalikuwa juu ya tukio la chumbani. Nilijiuliza kwa nini nimuone kunguru badala ya dada? Kwa nini imekuwa hivi? Huyo dada mwenyewe yuko wapi? Au hajafa? Kama hajafa yuko wapi basi? Sikupata majibu.

Wakati nikijiuliza maswali hayo, ghafla mlango wa chumbani ulifunguliwa. Nilielekeza macho mlangoni kumwangalia aliyetaka kuingia. Ajabu hakuna aliyeingia. Mlango ulikuwa vilevile umefungwa. Niliwatazama wenzangu kwa awamu lakini hakuna aliyejishughulisha na purukushani za mlangoni. Hawakusikia mlango ukigongwa au imekuwaje? Nilijiuliza.

Tukio hilo lilipita huku bado nikijiuliza kilichotokea chumbani bila majawabu. Nikiwa katika hali hiyo, ghafla mlango ulifunguliwa. Aliyeufungua aliingia chumbani taratibu. Sikujua alikuwa nani. Alikuwa anaingia taratibu sana na ajabu alikuwa amevaa nguo ndefu nyeupe ambayo ilimfunika mwili mzima. Kwa hiyo haikuwa rahisi kumtambua ni mtu wa namna gani, mwanaume au mwanamke. Nilimakinika kutaka kumjua. Hata hivyo, wenzangu hawakujishughulisha naye. Kila niliyemtupia macho alikuwa amejituliza. Hakuna aliyeangalia mlangoni.

Yule mtu alipoingia chumbani alikuja moja kwa moja nilipoketi. Aliponikaribia akajifunua ile nguo nikauona uso wake. Nilipiga kelele kwa hofu.
"Mamaaaa! Dada huyu, dada huyuu! Aaaghr!" Kelele zangu ziliwashtua watu waliokuwa chumbani. Waliniangalia. Wakati huohuo dada alipotea. Mlango ambao aliingilia dada na kuuacha wazi wakati ananifuata ulionekana umefungwa. Ulikuwa vilevile kama ulivyokuwa mara ya kwanza. Watu walinitazama kwa mchanganyiko wa mshangao na

huruma. Mama alinivuta kwake akanikumbatia kwa mapenzi makubwa. Nikatulia.

*** * ***

Siku iliyofuata ndiyo ilikuwa siku ya mazishi. Watu walikuwa wengi sana kila kona ya nyumba. Wingi wao ulikuwa kama siku ile ya ndoa. Tofauti za siku hizi mbili ni kuwa ile siku ya ndoa palikuwa na furaha sana na watu walizungumza kwa furaha. Leo ni huzuni na majonzi tupu. Hapakuwa hata mtu mmoja aliyeonesha dalili ya kucheka. Kadiri muda ulivyokuwa unasogea ndiyo watu walivyokusanyika. Mimi bado nilikuwa chumbani kwa mama pamoja na mama yake shemeji. Mlango ulifunguliwa akaingia shangazi.

“Jamani muda umefika wa kutia mwili wa marehemu kwenye jeneza. Mwenye kuhitaji kuushuhudia kwa mara ya mwisho aje huku chumbani,” alisema shangazi ambaye hakutaka hata kusubiri kuitikiwa au kukataliwa, akaondoka zake.
Mama alikuwa mtu wa kwanza kusimama na kuondoka. Mama yake shemeji alifuatia kisha watu wengine nami nikafuata nyuma. Nilijua kuwa huko haitokuwa kama wanavyomuona wenzangu. Tukiwa sebuleni kuelekea chumbani huko tulipishana na watu ambao walitokea huko chumbani kushuhudia mwili wa marehemu wakiwa na huzni kuu.

Kama tulivyotoka kule chumbani, ndivyo tulivyoingia chumba hiki; mama mbele, mama yake shemeji, watu wengine halafu nilifuatia mimi. Nilipoingia chumbani leo haikuwa kama jana. Ilikuwa zaidi ya jana. Wakati watu wakipishana kwenda kumuangalia dada pale kitandani, nilimuona akiinuka na kuja kwa kasi upande wangu. Mimba yake ilitangulia mbele huku mikono ameitawanya pembeni ishara ya kutaka kunikumbatia. Nilipiga yowe kubwa.

“Mamaaaa nakufaaaaa!” Ajabu pamoja na kupiga kelele ambazo zilisafiri kwa umbali wa mita hata mia moja hakuna hata aliyenisikia. Zaidi waliendelea kukizunguka kitanda kilicholazwa maiti huku wakitoa heshima zao za mwisho.
Umbali kutoka kitandani hadi pale niliposimama haukua mrefu. Ulikuwa kama hatua kumi au kumi na tano. Hata hivyo, dada alikuwa hanifikii japo alikimbia kwa kasi. Jambo lingine lililonishangaza zaidi ni kuwa pale kitandani watu waliendelea kutoa heshima zao za mwisho kuashiria kuwa mwili ulikuwepo pale. Kelele zangu za kuomba msaada huku nikitaja dada ziliishia kwangu mwenyewe. Hakuna aliyenisikia.

Watu waliendelea kutoa heshima zao kwa marehemu. Nilistaajabu sana. Niliendelea kusimama pale hadi akaja shangazi kunishika mkono. alinisogeza pale kitandani alipolazwa marehemu. Hapo nilikutana na kituko kingine. Nilipokifikia kitanda nilimkuta dada ameketi huku akilishikashika tumbo lake kwa matarajio ya kupata furaha zaidi siku chache zijazo. Aliponiona aliniashiria niketi karibu yake huku akitabasamu. Mambo hayo hakuna aliyeyaona zaidi yangu. Dada aliendelea kuniita nami nilikataa huku nikirudi nyuma taratibu.
Kurudi kwangu nyuma haikuwa dawa ya kumkwepa. Aliponiona namkatalia wito wake aliamua kunifuata. Nilipomuona amenikaribia, nilitimua mbio huku nikilia. Mbio hizo zilikomea chumbani kwa mama ambako nilikwenda moja kwa moja kujitupa miguuni mwake.
Sikufahamu nililala kwa muda gani. Nakumbuka nilikuja kuamshwa na rafiki wa marehemu. Baada ya kuniamsha aliniambia watu walishakwenda na kurudi makaburini na walishatawanyika muda mwingi. Waliobaki pale nyumbani walikuwa ndugu, jamaa na marafiki kwa ajili ya matanga.
“Mh!” Niliguna.

*** * ***

Sifa kubwa ya binadamu ni kusahau. Ukiwa hai waweza kusahaulika kwa muda, lakini ukakumbukwa kwa muda kadhalika. Ni vyema kumsahau aliye hai kwani ipo siku utamkumbuka hasa ukimuona. Kumsahau aliyekufa ni rahisi sana ila kumkumbuka kwake ni ngumu. Hata kama yapo mambo aliyoyafanya ya kukumbukwa au vitu alivyoviacha vya kukumbukwa hakulingani na anavyokumbukwa aliye hai. Kwa hivi, msiba wa dada ulikuwa ni sehemu tu ya kumbukumbu ya familia. Alikumbukwa mara chache akasahaulika mara nyingi.

Mwezi mmoja ulikatika. Habari zake zilikoma taratibu kuzungumzwa. Kumbukumbu ya matukio yote mawili zilianza kufutika katika bongo za watu. Mambo tofauti na matukio yale yalichukua nafasi. Hiyo ni kwa upande mmoja.

***ITAENDELEA***

# MIAMBA WA AFRIKA

## Samora Machel - 09

Hans Louw, mfanyakazi wa Ofisi ya Ushirikiano wa Kiraia, anadai kuwa alisaidia kuleta kifo cha Machel.[32] [33] Pik Botha, waziri wa mambo ya nje wa Afrika Kusini wakati huo, ambaye baadaye alijiunga na ANC, alisema kwamba uchunguzi kuhusu ajali ya ndege unapaswa kufunguliwa tena. [34]

Mwandishi wa habari wa Ureno, José Milhazes [pt], ambaye aliishi Moscow kuanzia 1977 hadi 2015 na kwa sasa [lini?] anafanya kazi katika gazeti la Ureno la Público na kama mwandishi wa kituo cha televisheni cha Ureno SIC, anashikilia kuwa ajali hiyo ya ndege haikuwa na la kufanya. kwa jaribio lolote au kutofaulu kwa mitambo, lakini ilitokana na makosa kadhaa ya wafanyakazi wa Urusi (pamoja na rubani), ambao, badala ya kutekeleza majukumu yao kwa bidii, walikuwa na shughuli nyingi za bure, kama vile kugawana vileo na vinywaji baridi ambavyo havikupatikana nchini Msumbiji. alikuwa na uwezekano wa kuleta kutoka Zambia. Kwa maoni ya Milhazes, mamlaka ya Usovieti na Msumbiji walikuwa na nia ya kueneza nadharia ya jaribio la serikali ya Afrika Kusini: Wasovieti walitaka kulinda sifa zao (wakiwaondolea ndege na wafanyakazi kutokana na jukumu lolote), Wasumbiji walitaka. kuunda shujaa.[35]



Hata hivyo, mwaka wa 2007, Jacinto Veloso, mmoja wa wafuasi wa Machel bila masharti ndani ya Frelimo, alisisitiza katika kumbukumbu zake kwamba kifo cha Machel kilitokana na njama kati ya maafisa wa siri wa Afrika Kusini na Soviet, ambao wote walikuwa na sababu za kumuondoa. . Kulingana na Veloso, balozi wa Usovieti aliwahi kumwomba Rais ahudhurie hadhira ili kuwasilisha wasiwasi wa USSR kuhusu kuonekana kwa Msumbiji "kuteleza" kuelekea Magharibi, ambapo Machel alijibu "Vai à merda!" (Nenda kuzimu!). Baada ya kumwamuru mkalimani kutafsiri, alitoka chumbani. Wakiwa wamesadiki kwamba Machel alikuwa ameondoka bila kubatilishwa kutoka kwenye obiti yao, Wasovieti walidaiwa hakusita kumtoa sadaka rubani na wafanyakazi wote wa ndege yao.

**Mazishi**

Mazishi ya kiserikali ya Machel yalifanyika Maputo tarehe 28 Oktoba 1986. Yalihudhuriwa na viongozi wengi wa kisiasa na watu wengine mashuhuri kutoka Afrika na kwingineko, akiwemo Dk. Robert Mugabe wa Zimbabwe, Dk. Kenneth Kaunda wa Zambia, Julius Nyerere wa Tanzania, Mfalme Moshoeshoe. II wa Lesotho, Daniel arap Moi wa Kenya na Yasser Arafat wa Jimbo la Palestina. Pia walikuwepo kiongozi wa ANC Oliver Tambo, bintiye Rais wa Marekani Maureen Reagan, Naibu Waziri Mkuu wa Kwanza wa Umoja wa Kisovieti Heidar Aliyev, na kiongozi wa haki za kiraia, Jesse Jackson.

Katika mazishi, kaimu kiongozi wa Frelimo, Marcelino dos Santos, alisema katika hotuba yake: "Mshtuko wa safari yako ambayo hakuna kurudi bado unatetemeka katika mwili wa taifa zima. Ulianguka katika mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi ... alielewa ubaguzi wa rangi kama tatizo la wanadamu wote."

Samora Machel alizikwa kwenye pango lenye umbo la nyota katika Meza ya Mashujaa wa Msumbiji, makutano ya trafiki huko Maputo.

**Mwisho**

**Katika Toleo lijalo, safu hii itakuletea Mwamba mwingine wa Afrika. Nani huyo?**

**Endelea kuwa nasi**

# SAKO KWA BAKO: SIMULIZI CLUB-Ilikotoka na inakoelekea...

**Katika safu yetu ya SAKO KWA BAKO leo tunaileta kwenu SIMULIZI CLUB. Hii ni platform inayogeuza fasihi andishi kuwa fasihi simulizi. Wao ni nani na wanafanya nini? Twende pamoja.**

**1– Unaweza kutueleza Simulizi Club ni kitu gani.. Ilivyoanzishwa na ilipofika na lengo lenyewe la uanzishwaji wake?**

Simulizi Club ilianzishwa mwezi January 2022. Nilianzisha kwa kuweka waandishi watano wawe wanapost kwenye kurasa (page) ya Simulizi Club kwa makubaliano maalumu.

Baadae tukajielekeza kwenye uzalishaji wa simulizi za sauti, hii ilikuwa ni baada ya kugundua simulizi kwa mfumo huu zitawafikia wengi hasa wale wavivu wa kusoma, walemavu wa macho, wasiojua kusoma pia hata wale watu wazima wenye matatizo ya uoni, na kadhalika.

Kama ujuwavyo, *almost* kila jambo huwa na mwanzo mgumu na ndicho kilichonitokea mimi.
Kuna wakati nilikaribia kukata tamaa kwa nikifanyacho sababu *support* niliyozani ntaipata toka kwa waandishi na wasimuliaji wangu, sikuipata kwa namna nilivyotarajia.

**2- Vipi mapokeo ya wananchi yakoje kuhusu mfumo huu wa kuwafikishia kazi za kifasihi?**

**Simulizi Club:** Mapokezi ya kazi zetu za sauti sio mabaya na ni ya kutia moyo ila kazi kubwa bado inahitajika.

**Asante nafikiri wasomaji wamepata picha fulani kuhusiana na Simulizi Club.
Sasa hebu tueleze changamoto gani unakutana nazo kwenye mradi mzima wa Simulizi Club?**

Hakikaaa... changamoto kuu hapa ni watu nilionao. Kwa sasa timu ya Simulizi Club tupo wanne jumla. Watatu ni wanaume na mwanamke mmoja.

Timu ina watu 4 ila kwenye utendaji ni mmoja...
So ushirikiano ni mdogo sana baina yetu. *As you know*, kidole kimoja hakivunji chawa... ila mimi kama muhusika mkuu, nazidi kulisongesha gurudumu licha ya kukosa ushirikiano wa maana.

**Mtu anapataje simulizi za Simulizi Club?**

**Simulizi Club:** Kwa sasa kazi zetu zinapatikana youtube, na hivi punde zitaanza kurushwa Facebook page ya Simulizi Club, kule X/Twitter, insta na kwengine kadri tutakapozidi kutanuka.

Yani mtu anatakiwa kwenda google au youtube kisha aandike Simulizi Club, watamletea kazi zetu zote.

**Simulizi Club:** Pia hapa whatsapp kuna kundi ambalo huwa natuma simulizi za sauti na ni bure kabisa kujiunga

**Asante Sana... Neno la mwisho wa wapenzi wa Simulizi Club…**

**Simulizi Club:** Wao ndio uti wa ukuwaji wetu. Waendelee kutusapoti na sisi tutazidi kuwaletea kazi kali kali... pia tunawapenda sana.

Haya ni mapinduzi makubwa sana katika uwanda huu wa fasihi duniani kote. Watu wa Simulizi Club wametuletea mfumo huu wa sauti ambapo riwaya zinaweza kulifikia kundi kubwa zaidi na kwa wepesi zaidi.

Ngurumo ya Mwandishi inakutakieni yote mema kabisa katika mapambano haya.

# KISASI CHA HISIA— 01

**MKASA: KISASI CHA HISIA**
**"Suprise ya maumivu"**

**Na. CRARENCY SANGA**

.....01.....

Ilikuwa kama ndoto iliyokuja kwa uhalisia kamili, sasa alikuwa anatazamana na kitu ambacho asingependa kijitokeze tena maishani mwake. Mara kadhaaa alijipiga piga kichwa kwa kudhani huenda ndoto na ataamka lakini haikutokea hivyo, lilikuwa ni jambo lililokuja katika uhalisia wake halisi

Mkononi alikuwa ameshika kadi ya mwaliko wa harusi, machoni alikuwa ameshachoka kuyafuta machozi sasa aliacha yatoke yenyewe bila utaratibu wowote ule. Zilikuwa zimepita dakika kumi toka awe amekaa eneo lile kabla ya kushituka kuwa yu kati kati ya uwanja na ni mchana wa jua kali

"Kumbe nimekaa kati kati ya uwanja na jua lote hili kali" alijisemea huku akiinuka na kupukuta vumbi makalioni kisha akapiga hatua tatu mbele

"Ina maana ulikuwa ni mpango wa mda mrefu, mbona kadi ya mchango sikupewa nimekuja kupewa ya harusi na lini ulikuwa uchumba au ameamua kunifanyia suprise" yalikuwa ni maswali yaliyokishambulia kichwa chake kwa wakati mmoja

Aliondoka eneo lile huku akiwa na mawazo lukuki yakikiambata kichwa chake. Huenda hakujua ni kwa nini haya yote yanatokea kipindi kifupi toka arudi kutoka chuo.

Alitamani apate walau wa kumsimulia maswahibu yaliyoujaza moyo wake kwa wakati huo lakini hakupata hata wa kumuamini tena. Alijihisi ni mtu asiye na bahati tena.

"Catherine umenifanyia SURPRISE YA MAUMIVU, naahidi nitakulipa katika yote hayo umenifanyia" aliongea huku akiwa anaichana ile kadi kisha kuviacha vipande vikizagaa chini.
________&&______



Ilikuwa ni harusi yenye kila sifa ya kuitwa harusi ya kifahari. Zilikuwa zimebaki siku tano pekee harusi ifanyike. Mji mzima ulikuwa umefunikwa kwa shangwe na nderemo. Shamra shamra za hapa na pale zilikuwa zikiendelea kuisubiri siku ya tukio lakini mambo hayakuwa sawa kwa mwanadada Dayana.

Huyu alikuwa amejifungia chumbani kwake kwa muda wa mwezi mzima akiwa anajitahidi kusahau maumivu ambayo hajui yataisha lini.

Ni mlio wa simu yake ndio uliokuwa umemtoa kwenye mawazo ambayo alikuwa amepotelea huko. Ni muda sasa toka aachane na mpenzi wake, amekuwa ni mtu wa kujishindia ndani na amenusurika kufa zaidi ya mara tatu kwa nyakati tofauti tofauti.

Mara ya kwanza alikunywa sumu lakini aliwahishwa hospitalini na alifanikiwa kupona. Mara ya pili na ya tatu, alijaribu kujiua kwa njia tofauti tofauti lakini alinisurika. Ni kama Mungu alikuwa anataka kumuweka aje ashuhudie adui zake wakiaibika.

Aliinuka na kwenda moja kwa moja kupokea simu iliyokuwa mezani. Aliichukua na kuangalia namba ya mpigaji kisha akaipokea na kuiweka sikikoni

"Hallow"Aliongea Dayana

"Unaendeleaje" sauti upande wa pili ulihoji

"Naumwa Enjo, naumwa hali yangu inazidi kudhoofika siku baada ya siku" aliongea Dayana

"Dayana, jitahidi utamsahau usiwe mnyonge hivyo wanaume wapo wengi utapata mwingine mzuri zaidi ya huyo, achana naye ameshaoa huyu na harusi yake inakaribia bado siku tano pekee hatuwezi kurudisha kila kitu nyuma maji yashamwagika haya Dayana" Enjo aliongea

"Sawa nimekuelewa ila hali yangu sio nzuri hata kula ni kwa tabu sana mimi ninaumwa najutia maamuzi yangu ya kumkabidhi imani yangu

# KISASI CHA HISIA — 01

kubwa kiasi kile na haya ndio matokeo" Dayana aliongea

"Achana naye wanaume wapo utapata atakayekupenda mwaya"

"Sawa ngoja mimi nipumzike Enjo" Aliiweka simu mezani kisha na yeye kurudi kwenye kitanda chake na kulala.

Saa zilisonga na siku nazo zikasonga hadi siku ambayo Dayana aliipokea simu iliyomuweka katikati ya faraja na huzuni simu ambayo hakutegemea kama itamtafuta.

Ilikuwa ni asubuhi ndipo Dayana aliona ujumbe mfupi wa simu ukiwa umetoka katika namba ngeni. Aliusoma ujumbe kwa makini walau amtambue aliyetuma lakini hakumpata hata alipopiga ile namba haikuwa hewani kwa wakati huo.

Ilikuwa ni sms iliyoandikwa "Habari Dayana, pole kwa wakati mgumu unaopitia ni kama moyo wako umevunjwa mara mia basi mimi wangu umevunjwa mara elfu, tumaini langu limepotea mchana wa jua kali bila huu moyo mgumu nilipewa na Mungu ningekuwa nishawekwa ndani ya janeza nimezipata habari zako kutoka kwa wasamalia wema  zimekitonesha kile kidonda kilichoanza kukauka sasa kinavuja damu tena.

Nikipata nafasi nitakuja kuongea na wewe Ijumaa kabla ya harusi yao nitakuja Dayana japo tufarijiane wakati fika nikiwa najua kipofu hawezi kumuongoza kipofu mwenzake,  mwenzako ni kama niliyepofuka uzeeni hii njia ninaijua nakuhakikishia nakuja kukuongoza" ni mimi steve ex wa mke wake ex wako.

Alimaliza kusoma ujumbe ule, hakutaka amjibu kwa sms muhusika bali alimpigia simu lakini kwa wakati huo namba ya muhusika haikuwa hewani tena basi shauku yake alikuwa ameielekeza Ijumaa kama muhusika alivyodai kwenye ujumbe alioutuma.

Hatmaye huwa wanasema usiku wa deni hauchelewi kukucha ndio ilivyokuwa kwa Dayana. Ijumaa ilikuwa imeshawadia na sasa alikuwa anausubiri ugeni uliokuwa umemuahidi kuja. Muda ulienda lakini hakukuwa na dalili zozote za mtu kuja hadi kufika saa nne usiku alikuwa tayari ameshakata tamaa na aliamua alale.

Nusu saa baadae simu yake ilimtoa kwenye usingizi. Aliamka kwa uchovu na kwenda kuipokea. Ilikuwa ni sauti moja iliyomwambia ya kuwa anahitajika nje akampokee mgeni

Ilikuwa ni sauti ngeni kabisa masikioni pake. Aliamka upesi upesi na kwenda kufungua mlango hapo akakutana na mgeni wake uso kwa uso.
Aliweza kutazamana na binadamu mrefu wa umbo na mwembamba kiasi. Kofia yake ya kumziba uso ilifanya asionekane vizuri  hadi pale alipoamua kuivua .

Ilikuwa ni sura ngeni kabisa machoni pake. Kwa mara ya kwanza anamuona mtu aliyewasiliana nae mara mbili tu na kuwa na shauku ya kumuona moja kwa moja.

"Nikaribishe ndani mbona tu unaniangalia tu Dayana" aliongea steve

 "Karibu"aliongea huku akimpisha Steve aingie

Nae steve aliingia na kupitiliza kukaa kwenye sofa, kisha akaelekeza macho yake kwenye television. Dayana alipaliza kuufunga mlango wake vizuri nae alirudi na kukaa kwenye sofa jingine.

"Mbona hujaniuliza nimepajuaje hapa kwako" aliongea steve

"Amna si umeelekezwa jamani kwani umefikaje" aliongea Dayana huku akitabasamu

"Pole sana nimeona huna tabasamu la furaha tena unalazimisha tabasamu la uchungu" aliongea steve kisha akaendelea

"Nimetoka kwenu  nimekukosa wamenambia ulikuwa unashida ya kuonana na mtu ndio maana umeamua uje kwako ni kweli" Steve

Dayana aliitikia kwa kutikisha kichwa kumaanisha ni kweli kabisa.

"Bila shaka mtu mwenye ni mimi si ndio"

"Ndio"

***ITAENDELEA...***

# RIWAYA: CRONOC 7 (07) – richard MWAMBE

*Ilipoishia*

**Akatoka nayo mpaka kwenye moja ya migahawa iliyo katika eneo hilo na kuingia ndani yake. Akaketi katika kona kabisa akihakikisha kuwaona wote wanaoingia na kutoka katika mgahawa huo. Lengo lake amgundue huyo anayemfuatilia, yaani mteja wake au kibaraka wake.**

---

*Endelea*

"Is dead!" daktari wa kike alimwambia mlinzi wa karibu wa tajiri huyo akimaanisha ameshakufa.

"Ah!" Yule kijana aling'aka na kujishika kichwa. Nimezidiwa akili! Akawaza huku akijitupa kwenye kiti na kushuhudia shuka safi jeupe likiufunika mwili wa bosi wake.
Safari yao iliishia kwenye jengo kubwa ambalo kwalo zilihifadhiwa maiti kwa malipo maalum. Helikopta ile ikatua na mwili wa Kumeil, tajiri wa Kihindi, mmiliki wa majumba kadhaa ya starehe katika jiji hilo. Hapo ukahifadhiwa. Ijapokuwa ilikuwa ni ngumu kuamini kinachotokea lakini Colbas alikuwa kamaliza kazi yake ndani ya saa zisizozidi kumi na mbili.

Habari hiyo haikuwa nzuri hata kidogo kwa swahiba zake ambapo asubuhi ya siku hiyo walikuwa pamoja katika kasri lake huko Kinangop na sasa wanapata taarifa kuwa mdau wa juu kabisa naye ameuawa.

Katika gari moja la kisasa, Hammer lenye vioo vya giza kulikuwa na watu wasiopungua watano, wote wakiwa kimya hakuna hata aliyefungua kinywa chake.

"Nini hiki?" mmoja akauliza huku akiivua miwani yake na kuiweka kando.

"Sielewi, sasa hali imekuwa mbaya hata siwezi kurudi nyumbani maana nina wasiwasi hata na mke wangu," mwingine akadakia. Kati yao kulikuwa na kijana ambaye alikuwa mlinzi wa kwanza wa Kumeil.


"Ilikuwaje ukamruhusu muuaji?" yule mzee akamuuliza kijana huyo.

"Kumeil mwenyewe alisema aruhusiwe baada ya kujieleza kuwa yeye ni SM wa Patrick Njuwe, nanyi mnajua umuhimu wa mjumbe huyo na kuwa ni mtu asiyejulikana. Nilimpekuwa mwenyewe na kila kitu aliacha pale langoni akaingia yeye na hiyo bahasha mkononi," akaeleza.

"Sasa ilikuwaje mpaka mtu huyo hamkumtia mkononi? Bila shaka ni yeye anahusika na mauaji yote yaliyotukia leo," yule mzee aliongea kwa uchungu sana. Yule kijana mlinzi wa Kumeil akatulia akivuta kumbukumbu ya tukio lile.

*** *** ***

Colbas alitulia tuli katika kiti cha uwanja wa ndege akisubiri kuondoka nchini hapo. Ndani ya ile bahasha aliyoikuta katika ndoo ya takataka kulikuwa na hundi ya pesa nyingi sana kama malipo yake na pia tiketi ya ndege ya kurudi kwao.
Kilichomshangaza ni mipango yote ilivyopangwa, maswali yaliyopita kichwani mwake yalikosa majibu. Kwa ujumla hakuwa na amani kwani alijua wazi kuwa mtu aliyemtuma kazi hiyo atakuwa anamwangalia muda wote. Aliamini hilo kutokana na jinsi mambo yote yalivyokwenda. Alijiuliza angempa vipi taarifa ya vifo hivyo, lakini kabla hajatoa taarifa alipigiwa simu iliyompongeza kwa kazi.
Hata kama wamepanga kuniua baada ya kazi wanaweza kufanya




hivyo muda wowote. Aliwaza huku akipepesa macho kumwangalia kila aliyepita mbele yake, labda angemgundua mtu anayemfuata kwenye nyendo zake hizo.

"…Abiria wote mnaoelekea Antananarivo mnaombwa kuingia ndegeni kwa kutumia mlango namba 48…"

Sauti nyororo ya mwanadada ilisikika katika vyombo maalumu vya kazi hiyo. Colbas akainuka na kunyanyua begi lake dogo huku lile sanduku akiwa kalikabidhi nalo limepakiwa kama mzigo katika ndege hiyo kubwa. Akajivuta na kupita katika mlango huo, alipoufikia akamkabidhi tiketi mwanadada aliyemkuta hapo, naye akaipokea na kuitazama, akatikisa kichwa juu chini.

"Welcome on board Sir," akamkaribisha huku akimpa ile tiketi na Colbas akapotelea ndani ya ndege hiyo tayari kwa safari. Mawazo yake yakaondoka kwa yule aliyefikiri anamuwinda na sasa yakabaki kwa mwanamke huyo aliyemkaribisha kwa bashasha za hali ya juu.

**SURA YA 03**

MISA ya jumapili ilikwisha. Askofu Bariki Zebetoni alitoka kanisani huku waumini wakimfuata huku na huko kumsalimia. Alipendwa sana kwa moyo wa ukarimu aliokuwa nao. Jumapili hii hakuwa na muda sana wa kuzungumza na watu wake, alikuwa akiwahi kuelekea katika jumba lake la ghorofa moja. Wale wachache waliokuwa na bahati walimpa japo mkono lakini wengine walipewa baraka tu. Baba huyo wa kiroho aliingia ndani ya jumba lake.

"Nahitaji kusafiri leo hii…" akamwambia mtawa wa kike aliyekuwa ameketi naye katika sebule kubwa ndani ya jumba hilo.

"Aah, mbona ghafla hivyo baba?" yule mtawa akauliza.

"Hapana siyo ghafla, ilikwishapangwa ila wewe hukuijua…" akamwambia huku akisimama na kuliendea jokofu, "… naomba ushughulike na kazi zote ambazo nimeziacha nitarudi baada ya siku nne tu," akampa maagizo na kuchukua maji baridi kwenye chupa ndogo. Alipotoka hapo akaingia ofisi nyingine na kukutana na kasisi aliyekuwa akikaimu nafasi yake endapo yeye anakuwa hayupo jimboni, wakaagana na kisha akaondoka zake kuelekea uwanja wa ndege.

*** *** ***

Katika maegesho ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa J.K Nyerere, Gina alishusha gazeti alilokuwa akilisoma, na kuliweka nusu ili kuyaruhusu macho yake kuona kile kinachotukia mbele yake. Kwa jicho hilo lililofunikwa na miwani iliyokuwa ikipiga picha ya video na kuisafirisha mpaka katika moja ya gari lililoegeshwa eneo hilo ambamo ndani yake Chiba alikuwepo, aliendelea kutazama hili na lile.

Wakati ulipofika akainuka kitini, akavuta hatua mpaka katika eneo ambalo wasafiri wanakutana kabla ya kuingia ndani, mbele yake alisimama Askofu Bariki Zebetoni. Gina akamfikia na kumsalimu kwa heshima huku bado miwani yake ikiwa inarekodi picha na sauti.

"Baba mbona unatuacha kondoo wako?" akamwuliza kwa utani.

"Aaaa! Mwanangu nipo safarini kidogo, kwani tuko pamoja?" akamjibu na kuuliza.

"Hapana mi naelekea Arusha," akamdanganya.

"Ok, mi niko njiani kuelekea London lakini siku nne zijazo nitarudi," akamjibu.

Gina akaagana na Askofu huyo na kujichanganya na watu wengine waliokuwa katika eneo hilo. Asubuhi hiyo Gina alikuwa katika kazi maalum, alikuwa akimfuatilia Askofu huyo kutokana na kuwapo na taarifa za sintofahamu za kiongozi huyo wa kiroho.

"Trip to London!" Gina akaongea huku akiwa kasogeza saa yake karibu na kinywa chake.

"Copy! Ukiangalia unamwona peke yake au ana kampani?" sauti ya upande wa pili ikauliza.

"No! bado naangalia lakini sioni dalili …"

"Abort … retreat!" ile sauti ikamwamuru Gina kusitisha kazi anayofanya na kurudi mara moja. Akaondoka eneo lile na kuelekea kwenye yale maegesho akihakikisha haonekani na mtu yoyote asiyemtaka.

"Welcome back," Chiba akamwambia Gina huku akiwasha gari na kutoka eneo lile, "hatua ya kwanza tumemaliza," akaongeza kusema.

"Sasa breki wapi?" Gina akatupa swali huku akiikunja ile miwani na kuiweka katika kikoba chake.

"Baraza la Maaskofu, kuna mtu wa kukutana naye pale," Chiba akamwambia Gina huku akichukua Barabara ya Pugu na kuelekea mjini.

"Huyu mzee ana nini hata tumfuatilie hivi?" Gina aliuliza.

"Just wait, utajua tu, TSA haiwezi kumfuatilia mtu kama hana tatizo, ukiona hivyo kuna jambo na jambo lenyewe utalijua tu," Chiba akaeleza.

"Lakini ni kiongozi wa dini yule…!"

"Gina - Gina … kuna viongozi wa dini wanavaa tu vazi hilo lakini ndani yao ni viumbe wengine kabisa…" Chiba akaeleza.

"Ok, nimekupata, kama ni hivyo hakuna wa kupona,"

"Hilo nalo ne …"

***ITAENDELEA***

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani mwezi wa November, 2023.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

**Ilipoishia...**
**"Angalia mume wangu!" alisema mke wa kassim, "Mke wa Alibaba alikuja kuniazima mizani ili akapimie nyama, mimi sikumuamini nikapaka asali chini ya mizani, na angalia sasa aliporudisha nikaona hii sarafu ya dhahabu imenata huku kwenye asali bila ya wao kujua, na ndio imenisaidia kujua walichokuwa wanakipima".**

**Endelea...**

Kassim alipoangalia kwenye ile mizani na kuona ile sarafu ya dhahabu alishtuka sana. "Mimi ni tajiri!" alisema Kassim "lakini Alibaba atakuwa tajiri kunishinda mimi, lazima niende nikamuulize amepata wapi dhahabu zote hizi, inaelekea ni nyingi sana mpaka anaamua kuzipima kwenye mizani!!". Hapana mume wangu" Alijibu mkewe,"Usiende sasa hivi ni usiku sana, wewe lala kwanza upumzike kisha kesho asubuhi ndio uende, lazima watuambie kila kitu, hawawezi kuficha siri hii". "sawa mke wangu nimekuelewa" alisema Kassim, "nitaenda huko asubuhi".

SURA YA PILI:

**KUINGIA MTEGONI**

Je Kassim alikuwa na furaha juu ya mafanikio ya ndugu yake? Hapana! Hakuwa na furaha bali ni wivu. Kassim hakulala usiku ule na alikuwa hafikirii chochote isipokuwa Alibaba na Dhahabu tu usiku kucha.

"Sio haki kabisa!" alijisemea Kassim. "Nimefanya kazi kwa bidii miaka yote hii kuhakikisha kwamba napata hela za kutosha, na mpaka sasa mimi ni tajiri, lakini Alibaba alikuwa kazi yake ni kukata kuni na kuuza mjini na kupata hela kidogo sana. Amepata wapi dhahabu hizi? Nani atakuwa amempa? Lazima nijue tu na mimi nipate za kwangu".

Jua lilipochomoza tu, Kassim aliamka huku amekunja sura. "Sio vizuri kabisa!" Alisema. "nitaenda kuzungumza naye nijue kila kitu, ndugu hawawezi kufichiana siri kiasi hiki."

"Vizuri sana!" alijibu mke wake. "Tena nenda na ile mizani ukamuoneshe sarafu ya dhahabu iliyonata kule chini, hii itasaidia kumfanya atambue kwamba tumeshagundua siri zao."

"Hilo ni wazo zuri!" alisema Kassim. "kwahiyo nenda jikoni kailete haraka niwahi huko."

Basi Kassim kwa mwendo wa kasi na wa tamaa kubwa sana kama mtu anayewahi sehemu fulani muhimu sana, alivuka mtaa wa pili mpaka kwa kijijumba kidogo cha ndugu yake Alibaba, kisha akapiga hodi.

Alibaba akaja kumfungulia na ikawa ni ajabu sana kumuona kaka yake pale.

"Habari yako, Kassim". Alisalimia Alibaba. "Tafadhali ingia ndani na uniambie mbona ni asubuhi sana upo hapa kwangu?"

"Najua siri yako, Alibaba!" alijibu Kassim. "Unasema kwamba wewe ni masikini mkata kuni, lakini kumbe una dhahabu nyingi sana mpaka unazipima! Umezipata wapi ndugu yangu?"





Alibaba akajifanya kama hajui kitu na kushangaa. "Dhahabu?" alisema Alibaba. "una maana gani? Mimi sina dhahabu, mimi ni masikini kama unavyonijua, mimi naenda msituni kila siku kukata kuni, tajiri hafanyi hivyo, ningekuwa tajiri ningekuwa na maisha mazuri, ningekaa katika jumba kubwa la kifahari, ningekuwa nakunywa maziwa na asali"

Baada ya Alibaba kumaliza kusema hayo, Kassim alinyanyua ile mizani usawa wa uso wa alibaba na kutabasamu. "Mkeo aliazima hii jana" Kassim alimwambia Alibaba.

"Alisema kwamba alitaka akapimie nyama. Mke wangu alishangaa sana kusikia hivyo, alijua kuwa nyinyi ni masikini sana hamuwezi kununua nyama, hivyo alipata hamu ya kujua kama kweli ni nyama basi ni ya aina gani, hivyo akapaka asali chini yake ili kipande kidogo kikiganda ajue ni nyama ya aina gani mlionunua.




**VITABU:**

**Jipatie vitabu pendwa vya riwaya tamu za kijasusi. MPATANISHI na HARUFU YA KIFO kutoka Jamvi la Simulizi. Vilivyoandikwa na mwandishi wako wa siku zote ambaye hana maneno mengi ila kalamu yake itakuonesha ubora wake.**

**Wahi sasa katika sehemu elekezwa ili ujipatie chako.**

**MPATANISHI—12,000/= na HARUFU YA KIFO—12,000/=**

**Aidha tunauza nakala laini ya vitabu mbalimbali vya riwaya za kijasusi. Usiwe mpweke, fanya uwezalo ukamate nakala yako.**









# SHUBAKA LA VITABU

**Katika Safu yetu ya SHUBAKA LA VITABU leo tutawaletea Maktaba kumi (10) bora duniani. Je; wazijua hizo. Karibu uwe nasi upate kujua haya,**

Sote twajua kwamba, maktaba ni sehemu au jengo linalotumika kuhifadhi nyaraka muhimu na vitabu kwa ajili ya watu kujipatia maarifa anuai. Kuna maktaba za taifa, mkoa, majimbo, wilaya, vyuo, shule na hata za binafsi.

Leo basi ningependa kuwajuza Maktaba kumi kubwa duniani ni zipi na zimehifadhi nyaraka kiasi gani. Tunaanza kutoka moja kwenda kumi.

## 1. MAKTABA YA UINGEREZA (British Library)

Maktaba ya Uingereza (British Library) ni maktaba ya kitafiti inapatikana jijini London. Hiyo ndiyo maktaba ya taifa. Inakadiriwa kuhifadhi nyaraka kati ya Milioni 170-200 kutoka nchi mbalimbali. Ilianzishwa tarehe 1 Julai, 1973.

Katika nyaraka zilizohifadhiwa ni pamoja na vitabu, majarida, magazeti, sauti na rekodi za muziki, ramani, stempu, michoro, miswada nk. Bajeti ya maktaba hii inakadiriwa kufikia Pauni za Kiingereza Milioni 142 ambazo ni sawa na Shilingi za Kitanzania 436,753,427,164.91. hii ni maktaba ambayo kila mmoja anaruhusiwa kwenda kuchota maarifa.

## 2. MAKTABA YA CONGRESS (LOC)

Hii ndiyo maktaba ya pili kwa hadhi ulimwenguni. Ilianzishwa mwaka 1800 na inahudumia watu wote. Ipo huko Marekani katika jiji la Washington DC. Ni maktaba ya taifa inayotoa huduma za kitafiti. Ina nyaraka zinazokadiriwa Milioni 173 za mifumo tofauti. Na ina zaidi ya wafanyakazi 3000.

Bajeti yake inakadiriwa kuwa ya Dola za Kimarekani milioni 802.128

Hii ndiyo maktaba kongwe kabisa ulimwenguni. Ndani yake vinapatikana nyaraka kama rekodi za sauti, vitabu, ramani, michoro, picha, miswada ya kisheria na hakimiliki mbalimbali. Ni ya wazi na hutembelewa na watu wote.

**Picha:**
**Kushoto– Maktaba ya Uingereza**
**Kulia– Maktaba ya Congress (Marekani)**





# KITABU NILICHOSOMA

**Anna Mbise Mobile Library**

**Jina la kitabu:**
***PEPONI***

**Jina la mwandishi: ***
**ABDULRAZAK GURNAH***

**Jina la msomaji:**
**FORO FOROY**
**Mkoa: Dar es Salaam**

**Niliyojifunza:**

✓ Uzuri wa afrika kabla ya ukoloni, na jinsi ukoloni ulivyoweza kuharibu tamaduni adhimu za kiafrika. Maisha asilia ya afrika yalikuwa mazuri na yenye maana, tofauti na upotoshwaji ulionezwa na wakoloni.

✓ Umuhimu na thamani ya uhuru. Uhuru ni lulu isiyopaswa kuchezewa. Mtoto Yusuf anapoteza uhuru wake kwasababu ya utumwa wa madeni ya baba yake. Madeni yanaweza kumfanya mtu awe tayari kufanya lolote bila kujali madhara/athari.

✓ Changamoto za makuzi na balehe kwa vijana. Balehe ni kipindi chenye majaribu mengi kwa vijana. Umakini na miongozo ya mara kwa mara inaweza kuwasaidia.

✓ Athari za ukoloni katika siasa, uchumi na tamaduni za waafrika. Matatizo na changamoto nyingi tunazoendelea kupambana nazo leo afrika, ni matokeo ya ukoloni mkongwe.

✓ Umuhimu wa kulinda familia zetu. Ugumu na ubaya wa kutengana/kupotezana na familia zetu. Yusuf alipoteza familia yake, tamaduni zake na historia yake kwa ujumla, na kuanza maisha mapya ugenini.


✓ Umuhimu wa kujisimamia kifikra na kufikia uhuru wa kweli. Kuna mstari unasema, wanaweza kukufunga pingu, kukutia gerezani, kukunyang'anya nk. Lakini uhuru wa kweli ambao ni uhuru wa kifikra, hauwezi kunyakuliwa na mtu yeyote.

✓ Majaribu na namna ya kuyashinda. Mke mwenye tabia za ajabu, wa mfanyabiashara Aziz, anamuingiza mtegoni kijana Yusuf kwa kumtaka kimapenzi. Yusuf anatoa somo la uthabiti na uaminifu.

✓ Mazingira yanavyoweza kumbadili mtu. Yusuf alikuwa kijana mwema asiye na hatia, lakini taratibu mazingira yalimbadili na kumjengea haiba tofauti.

✓ Kwa ujumla nimeipenda falsafa ya mwandishi ambayo kimsingi imejikita katika madhara ya kuparanganyika kwa familia, madhara ya kuishi nchi za ugeni, madhara ya utumwa na ukoloni, na ahadi hewa za viongozi/nchi zetu.Nashukuru kupata bahati ya kusoma kitabu hiki. Kina mafundisho mengi kwa jamii kuhusiana na historia yetu, tunu zetu na tamaduni zetu ambazo mwandishi anazifanisha na Paradiso iliyokuja kuharibiwa na ukoloni.

Tukitafute, tukisome






**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wailiana nasi kwa simu (call & Whatsapp) 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

**MAISHA NI YA THAMANI.**
**Na Jane Davis**

Nduzangu wasalaamu,balozi nasalimia.
Nami nashika hatamu,kapenini naingia.
Kwa kutumia kalamu,jamii kuifikia.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

Mweshimiwa Baruani,mheshimiwa Abwao.
Roghat nae vitani,nazitoa heko kwao.
Wamekuwa namba wani,kupaza sauti zao.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

Kakutenda Kuluthumu,kakukimbia Mrisho.
Mwenye ukajihukumu,na maamuzi ya mwisho.
Ati uimeze sumu,ndugu sio suluhisho.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

Shilingi kuwa adimu,njaa hodi inabisha.
Upambane kujikimu,hali ngumu ya maisha.
Usijitie wazimu,uhai kuukatisha.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

Kujiua ni haramu,zimetuusia dini.
Vyema wone watalamu,wakutibu akilini.
Pumziyo mwanadamu,ni thamani ithamini.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

Nina ombi sio gumu,kwa tukufu Serikali.
Pawe tume maalumu,kwenye kanda mbalimbali.
Janga hili lisidumu,tukalipinge vikali.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

Dakitari waalimu,watalamu wa Akili.
Tuieneze ilimu,liondoke janga hili.
Afya akili muhimu,unyongofu kuhimili.
Na kuishi ni thamani, usikatishe uhai.

**©Jane Davis**
**Mshairi & Balozi WWU Akili Platform Tanzania.**
**0626 551 859 kuingia kundini**
**Nzega Tabora.**

**#kuishinithamanikampeni**

**NIMEKUCHOKA**
Hutakati hukauki,
Michezoyo hauchoki,
Bilinganya na iriki,
Kwako mwamba sitoki.

Zoba umenigeuza,
Kama mkia wa chaza,
Ngoma zako nazicheza,
Ujinga nimeumeza.

Sijui ndiyo limbwata,
Mana kila siku wabwata,
Mambo yako Kama bata,
Buza mpaka Tabata.

Yahilahi Mola wangu,
Ulonipa si wangu,
Kama wangu vyaliwa vyangu,
Nikiona kwa macho yangu.

Mnyonge mnyongeni,
Haki yake mpatieni,
Waliyanena waneni,
Walipochoka umaninuni.

Uitwe mrembo gunia,
Au kinyama kwa njia,
Maana huna hisia,
Popote unatulia.

Iwe kwa Mzee twende,
Hujali hata Kaswende,
Unaliwa Kama tende,
Wakuua kifo Cha mende.

Hukomi lokupata,
Kipigo kukipakata,
Kujitapa kwakakata,
Wenye mali wakakata.

Hakika wewe si mtu,
Huba limejaa kutu,
Mejaa uchafu kuntu,
Kinena kwa ukurutu.

10. Nimekuchoka!
**Shujaa Maneno 'ulimi wa moto'**

# Habari Picha



Happy Birthday Rais wa UWARIDI
Hussein Issa Tuwa 'O6 November'



Abdulrazak Gurnah akisaini vitabu vya wasomaji




Kitabu cha TAMARA kikiwa kimefikishwa kwenye kilele cha Uhuru, Kilimanjaro

**Ukilipata jarida hili, mtumie na mwenzako.**

**"Tuambukizane furaha kwakuwa siyo ugonjwa"**
**by Luvanda Vitenge**

# ELIMU JAMII: Unaijua mimea inayokula nyama?

**Kutoka Facebook**

**MIMEA INAYOKULA NYAMA**

The meat-eaters of the plant world Inastaajabisha sana. Lakini ndivyo ilivyo. Habari juu ya mimea inayokula nyama (Carnivorous plants).

Tunaweza kusema nini kuhusu mimea ambayo, inawinda, inatega na kula wanyama ili kupata virutubisho vya kuifanya iendelee kuishi. Ni kama ambavyo tunashuhudia wanyama walao wanyama wengine, halikadhalika na mimea hii hufanya vivyo hivyo. Kuna spishi zipatazo 630 za mimea ya namna hii ambazo zimetambuliwa kisayansi. Japokuwa aina nyingi za mimea ya namna hii hutega na kula wadudu, lakini ipo ile ambayo ni mikubwa yenye uwezo wa kumeng'enya wanyama wenye ukubwa wa wastani ikiwemo mijusi. Mimea mingine ya aina hii hula viluilui vya mbu, bakteria na hata samaki.

Hata hivyo haimaanishi kwamba mimea hii hutegemea zaidi kula wanyama kama njia ya kuishi, na ulaji wa wanyama haumaanishi kwamba mimea hii inaacha njia zake za asili za kuishi na kwa kutumia mwanga wa jua, maji na hewa ya kaboni (photosynthesis) na mfumo wa mizizi bali ulaji wa viumbe hai hasa wanyama ni sehemu ya kutumia vizuri mlo unaopatikana.
Mimea hii hupatikana mahali tofauti kutegemeana na spishi husika lakini nyingi zinapatikana katika maeneo yenye unyevunyevu, kwenye mabwawa, vyanzo vya maji, pembezoni mwa vijito, misituni na hata kwenye miamba. Mimea hii inapatikana katika mabara yote ulimwenguni isipokuwa Antaktika.

Mojawapo ya spishi kubwa zaidi ya mimea hii ni ile inayopatikana jirani na kilele cha Mlima Victoria, katika kisiwa cha Palawani huko Ufilipino. Attenborough's pitcher plant, ni moja ya mimea iliyo hatarini kutoweka, hii ni kati ya mimea mikubwa zaidi ikiwa na urefu wa mita 1.50 na ikitengeneza 'maua' mfano wa bakuli lenye kipenyo cha hadi sentimeta 30, ambao ni ukubwa wa kuweza kabisa kudaka na kumeza wanyawa wadogo jamii ya panya.

Maua haya yanauwezo wa kuvutia na kuhadaa wanyama ambao hujikuta wanaingia mtegoni na kumezwa, kwa yenyewe kutoa harufu ya kuvutia ya nekta huku yakiwa na rangi ya kuhadaa ya maua ya kuvutia.

Spishi nyingine za mimea ilayo wanyama hujibadili rangi ili kuhadaa mawindo yao na hivyo wanyama hujikuta wakiwa tayari mtegoni pindi wanapoyasogelea. Kwa sababu ya rangi yake, wanyama kama ndege na wengineo hudhani wameona maua mazuri ya kujipatia nekta lakini kiukweli ni majani yaliyokaa tayari kudaka mawindo.

Mimea hii hata hivyo ina namna ya kipekee na ya kushangaza sana. Haidaki wala kula viumbe wengine wanaofanya uchavushaji, kwani huzalisha maua ambayo wadudu wachavushao huweza kuendelea na shughuli yao kama kawaida. Maua haya hujitokeza mbali ili mimea isije ikawatia mtegoni kama ilivyo kwa wanyama wanaowataka.
Swali la kujiuliza pengine ni kwa namna gani mimea huweza kula wanyama. Mara baada ya mnyama kudakwa na kuingizwa ndani ya mmea kupitia 'bakuli', mmea hutoa kimeng'enyo kinachoyeyusha chakula na kukifanya kuwa majimaji ambayo hutumika kama kirutubisho.

Japokuwa kuna spishi nyingi sana lakini karibu zote zina namna inayofanana ya kukamata mawindo yao, ikiwemo kutega, kutoa majimaji ya kunata (ulimbo), kitanzi, kung'ata, na kufyonza.
Mbinu zote hizi hufanyika kwa njia ya kumhadaa mnyama ili aweze kuingia ama kusogelea 'bakuli' kabla hajanyakuliwa.


Ukidhani kwamba umeona majabu mengi basi, haya ya leo yatakutosha kukupa mshangao.

**Wasalaam**
**Mudiri wa Korogwe.**
**9 Novemba 2023**
**Morning Site, Uluguru Mountains**




# Tangazo

















www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com